

Jina.....  
Shule.....

Nambari.....  
Sahihi.....  
Tarehe.....

**102/3**

**KISWAHILI**

**KARATASI YA 3**

**(FASIHI)**

**JULAI/ AGOSTI**

**Muda : saa 2½**

**MTIHANI YA PAMOJA WA WILAYA YA MANGA -2012  
CHETI CHA KUHITIMU ELIMU YA SHULE YA UPILI**

**102/3**

**KISWAHILI**

**KARATASI YA 3**

**(FASIHI)**

**JULAI/ AGOSTI 2012**

**Muda : saa 2 ½**

**MAAGIZO KWA MTAHINIWA**

- (a) Jibu maswali manne pekee
- (b) Swali la kwanza ni la lazima
- (c) Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki ; yaani : Riwaya, Tamthlia, Ushairi na Hadithi fupi.
- (d) Usijibu maswali mawali kutoka sehemu moja.
- (e) Kila swali lina alama 20.
- (f) Mtihani huu una alama 80.

*Karatasi hii ina kurasa 8 zilizopigwa chapa*

*Watahiniwa wanastahili kuona kuwa maswali yote yako na hakuna yaliyoachwa*

### **SEHEMU A:FASIHI SIMULIZI**

1. (a) Nini maana ya Miviga? (al.2)
- (b) Fafanua sifa zozote tano za miviga kashi ueleze dhima yake katika jamii (al.10)
- (c) Elezea sifa zinazotambulisha muundo wa nyimbo (al.8)

### **SEHEMU B.Utengano S.a Mohamed.**

2. Huko ukitolea mifano kutoka kitabuni, elezea migogoro mbalimbali inayojitokeza katika riwaya ya utengano. (al.20)
3. Mabadiliko sasa, alisema kwa kinywa kipana, kasha-----
  - (a) Fafanua muktadha wa dondo hili (al.4)
  - (b) Taja na uelezee tamathali ya usemi inayojitokeza katika dondo hili. (al.3)
  - (c) Mbali na mhusika anayerejelewa katika dondo hili, taja wahusika wowote wawili kisha uelezee mabadiliko yaliyowapata.

### **SEHEMU C: Kifo Kisimani .K Mberia**

4. (a) Thibisha kauli kuwa mwandishi wa tamthilia ya kifo kisimani amefaulu katika kutumia mbinu ya jazanda.
- (b) Kwa kutolea mifano mwafaka onyesha ufaafu wa anwani ‘Kifo Kisimani’ ukirejerea tamthilia husika (al.14)

### **SEHEMU D.Mayai Waziri wa Maradhi na hadithi nyingine K.W Wamitila**

5. Mwanamke amesawiriwaje katika hadithi zifuatazo
  - (a) Uteuzi wa moyoni
  - (b) Ngome ya nafsi
6. Hadithi ya Mkimbizi ni kioo cha matukio yanayotokea katika nchi za kiafrica. Fafanua athari za vita vya kikabila kwa mujibu wa hadithi hii.
7. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yanayofuata  
Mkata ni mkatika, haridhi hatoridhiwa  
Sina ninaloshika, wala ninalochukuwa  
Mlimwengu kanipoka, hata tone la muruwa  
Mrithi nini wanangu?

Sina ng'ombe wa mbuzi ,sina konde sina buwa

Sina hata makazi,mupasayo kuyajua

Sina mazuri makuzi, jinsi nilivyoachwa

Mrithi nini wanangu?

Sina kazi sina bazi, ila wingi wa shakawa

Sina chembe ya majazi,mno nikukamuliwa

Nikwa'cheni upagazi, ngumu kwenu ku'tuwa

Mrithi nini mwanangu?

Sina sikuachi jina,mkata hatasifiwa

Hata nifanye la mana,mno ni kulaumiwa

Poleni wangu sana, sina kwenu cha kutowa

Mrithi nini mwanangu?

Sina leo sina jana ,sina kesho kutwaaliwa

Sina zizi sina shina, wala tawi kuchipuwa

Sina wanangu mi sina,sina la kuacha kuraduwa

Mrithi nini wanangu?

Sina utu sina haki,mila yangu meuliwa

Nyuma yangu ili dhiki, na mbele imekaliwa

N'nawaua na miliki,hadi nitakapofukiwa

Mrithi nini wanangu?

Sina ila kesho kwenu,wenye kulongowa

Muwane kwa nyingi mbinu,Mwende pasi kupumuwa

Leo siye kesho yenu,kama mutajikamuwa

Mrithi nini wanangu?

(a) Kwa kuzingatia kibwagizo ,hili ni shairi gani? (al.2)

(b) Eleza sababu ya mtunz kutoweza kuwarithisha wanawe (al.3)

(c) Andika ubeti wa nne kwa lugha ya nathari (al.4)

(d) Dondoa mifano miwilimiwili ya

- (i) Inkisari (al.4)
- (ii) Tabdila (al.4)
- (e) Chambua shairi hili kiarudhi (al.5)
- (f) Eleza maana ya vifungu hivi (al.2)
  - (i) Mlimwengu kanipoka
  - (ii) Sinaconde sina buwa